**Geoffrey Goliama Simon, (1964 – 2015)**

Geoffrey Goliama Simon alikuwa mchungaji, mwalimu, na msimamizi wa kanisa nchini Tanzania.

**Maisha ya Awali:**

Geoffrey Goliama Simon alizaliwa nchini Tanzania Juni 18, 1964, katika familia ya Simon Goliama na Catherine Mpogolo, akiwa mtoto wa nne kati ya watoto saba. Watoto wengine waliozaliwa pamoja na Geoffrey ni: William, Monica, Annett, Geoffrey, Edward, Flora, na Jenny.

**Elimu, Kazi, na Ndoa:**

Mchungaji Simon alimaliza Shule ya Msingi Igurusi mwaka 1979, na kujiunga na Shule ya Sekondari ya Malangali ambapo alihitimu mwaka 1983, na kwenda kwa elimu ya juu kwenye Shule ya Sekondari Mazengo mwaka 1986. Mwaka 1987 alijiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mafunzo ya lazima ya kijeshi katika Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa ya Oljoro, Arusha.

Simon alianza masomo yake katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Januari 1989, ambapo alibatizwa katika Kanisa la Waadventista Wasabato Januari 27, 1990. Alipokataa kuhudhuria masomo na kufanya mitihani siku ya Sabato, alifukuzwa chuo kikuu. Baada ya hapo alikubali mwito wa kanisa kufundisha katika Shule ya Sekondari ya Parane Adventist, kuanzia 1991 hadi 1995.

Mwaka 1995 Mchungaji Simon alianza kusoma na Chuo Kikuu cha Griggs, kilichopo Marekani, kilichokuwa kinaendesha elimu ya chuo kikuu katika Chuo cha Waadventista Tanzania, Arusha. Alihitimu Shahada ya Kwanza ya Teolojia mwaka 1998. Alipomaliza masomo yake, alihudumu katika nyadhifa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuhudumu kama Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Suji Adventist kuanzia Mei 1998 hadi Aprili 1999. Januari 17, 1999, Mchungaji Geoffrey Mbwana alifunga ndoa ya Simon na Theresia Maira. Baadaye Simon na mkewe Theresia walipata watoto watatu, Catherine, Simon, na Caroline.

Simon aliwahi kuwa mchungaji wa Mtaa wa Njiro kuanzia Mei 1999 hadi Februari 2000. Kuanzia Machi 2000 hadi Machi 2005 aliwahi kuwa mwalimu mkuu wa Shule ya Sekondari ya Parane, na kuanzia Aprili 2005 hadi Desemba 21, 2005, alihudumu kama Mwenyekiti wa Konferensi ya Mashariki mwa Tanzania.

**Mauti**

Mchungaji Simon alikuwa miongoni mwa viongozi wanne wa kanisa hilo pamoja na dereva mmoja waliofariki dunia katika ajali ya gari ya kugongana uso kwa uso iliyotokea Desemba 21, 2015. Walikuwa wakisafiri kutoka makao makuu ya Konferensi Morogoro kuelekea Dar es Salaam kuhudhuria ibada ya mazishi ya Dk Witson

Mwamakamba. Viongozi wengine waliofariki katika ajali hiyo ni Mchungaji Loitopuak Lebabu, Katibu mtendaji wa konferensi; Mzuma Wikahi, Mweka Hazina wa Konferensi; Mchungaji Joshua Kulwa, mhadhiri wa theolojia katika Chuo Kikuu cha Arusha; na William Kulwa, dereva wa konferensi wa wakati huo, ambaye pia alikuwa mtoto wa Mchungaji Joshua Kulwa.